# Utangulizi: Chekechea – mwanzo bora






## UTANGULIZI: CHEKECHEA – MWANZO BORA

Chekechea ni shughuli ya kielimu ambayo inachukua mahitaji ya watoto kwa utunzaji, kucheza na kujifunza, na ni hatua ya kwanza katika elimu. Watoto wengi kwenye umri wa mwaka mmoja hadi sita ambao wanaishi Norway wanashiriki katika chekechea.

## CHEKECHEA – Utuoaji wa elimu kwa ushirikiano wa karibu na wazazi

Chekechea zote, za kibinafsi na za manispaa, hufuata Sheria ya Chekechea. Katika chekechea kuna walimu wa chekechea walio na kiwango cha elimu isiyo chini ya miaka mitatu ya vyuo vikuu. Hii inamaanisha kuwa mtoto wako anatunzwa na wafanyikazi wenye ustadi na wanaojali, ambao wana maarifa mengi kuhusu watoto. Ufuatiliaji wa mtoto hufanyika kupitia mawasiliano ya karibu na nyumbani. Unaweza kuzungumza na wafanyikazi kuhusu mambo ambayo unajiuliza, na pia unaweza kutoa mchango ambao unachangia ustawi na maendeleo ya kijamii ya mtoto wako. Mawasiliano kati ya chekechea na wazazi nyumbani ni muhimu sana wakati tamaduni tofauti zinakutana.






## CHEKECHEA – mahali pa kuchezea, kujifunza na maendeleo

- **Katika chekechea, mtoto wako anajumuishwa katika mazingira ya kijamii na watoto wengine.** Watoto wanajua tamaduni za kila mmoja, lugha na masilahi. Mtoto hujifunua na kujifunza kupitia mchezo na shughuli katika mwingiliano na watoto wengine na watu wazima. Mtoto hupata marafiki, huendeleza ustadi wa kijamii, na kupata uzoefu wa shule ya mapema ambao huimarishika katika maeneo yote ya maendeleo.
- **Ukuzaji wa lugha ya watoto hupata nguvu katika chekechea.** Kupitia michezo na kutafiti pamoja na wengine, watoto hukabiliana na mawazo, maoni, hisia na uzoefu wao. Hivi ndivyo mtoto huendeleza lugha yake katika chekechea.
- **Watoto wanaweza kujifunza lugha kadhaa kwa wakati mmoja**. Chekechea, pamoja na wazazi, lazima watumike pamoja ila wawezeshe mtoto kujifunza lugha ya asili na lugha ya kinorweji - lugha ya kiasili nyumbani na kinorweji katika chekechea.
- **Kujifunza lugha kunachukua muda.** Utafiti unaonyesha kwamba inachukua kutoka mwaka mmoja hadi mitatu kujifunza lugha vizuri ya kutosha kuweza kuwasiliana na wengine, na miaka mitano hadi saba kutumia lugha hiyo katika hali rasmi za ujifunzaji, kama vile kusoma na kuandika. Kwa hivyo, kuanza kuanza chekechea mapema ni muhimu ili kujifunza lugha ya kinorweji kabla ya kuanza shule.

## CHEKECHEA- hutoa fursa kwa wazazi

- Wakati mtoto wako anatunzwa na wafanyikazi wenye ustadi na wanaojali katika chekechea, hii inakupatia wewe kama mzazi nafasi ya kuanza kufanya kazi au kuchukua elimu.



# Je! nafasi ya chekechea hugharimu pesa ngapi?

Huku Norway, kuna bei ambayo imewekwa ya juu ya nafasi ya chekechea. Hii inamaanisha kuwa chekechea haziwezi kudai malipo zaidi kwa wazazi kuliko bei ile iliyowekwa kila mwaka na bunge. Zaidi, unapaswa kulipa pesa ya chakula.

Gharama hii hutofautiana kidogo kutoka chekechea hadi chekechea.

Bei ya nafasi ya chekechea inaweza kupatikana kwenye tovuti hii:
www.bergen.kommune.no/pris-barnehageplass.

Familia zenye mshahara wa chini zinaweza kuwa na haki ya kupunguziwa malipo ya chekechea.

Soma zaidi hapa kuhusu/malipo/bei: www.bergen.kommune.no/redusert-foreldrebetaling.

# Chagua chekechea na utume maobi ya nafasi ya chekechea:

Unaweza kuomba nafasi ya chekechea kwenye tovuti hii:
www.bergen.kommune.no/barnehageplass

Katika programu ya matumizi ya dijitali (kifungo cha bluu) unaweza kupata chekechea karibu na mahali unapoishi.

Maelezo ya jumla ya chekechea zote za Bergen zinaweza kupatikana kwenye tovuti hii:
www.bergen.kommune.no/barnehager.

Unaweza kutafuta chekechea katika eneo lako katika: www.barnehagefakta.no.

## Unahitaji msaada wa kuomba nafasi?

Tembelea Huduma ya Raia huko Kaigaten 4, mbele ya Byparken, au piga simu **55 56 55 56**. Hapa unapata pia usaidizi wa kuomba nafasi ikiwa hauna nambari ya kijitambulisha ya Kinorweji.



Picha: Kristin Hauge

*Huduma kwa raia Kaigaten 4.*

# Kuhusu kuwa mzazi katika chekechea



Picha: © Asle Bentzen

# USHIRIKIANO KATI YA CHEKECHEA NA NYUMBANI

Ili watoto wafurahie na kujiendeleza, ni muhimu kuwe ushirikiano wa karibu baina ya nyumbani na chekechea. Mkazo mkubwa umewekwa katika Sheria ya Chekechea na kanuni za mpango wa utaratibu na majukumu ya chekechea. Ili kufanikiwa kwa ushirikiano mzuri, ni lazima wazazi na chekechea wawe na mawasiliano ya karibu. Mawasiliano haya hufanyika kila siku kupitia upelekaji na uchukuaji wa watoto na pia mazungumzo ya maendeleo na mikutano ya wazazi.

## Mwanzoni

Mkutano wa kwanza na chekechea ni muhimu kwa familia na wafanyikazi. Chekechea itapanga ili kuwezesha mtoto na wazazi wapate usalama na uaminifu kutoka siku ya kwanza. Watoto ni tofauti, na wana njia toafauti za kuzoea kuanza chekechea. Wengine wanapata usalama haraka kwenye mazingira mapya, wakati watoto wengine wanahitaji muda zaidi wa kuzoea chekechea.

Mwanzoni, mtoto anapaswa kuwa kwenye chekechea kwa masaa machache, pamoja na mzazi mmoja au wote wawili. Hatua kwa hatua, idadi ya masaa inaweza kuongezwa. Chekechea itakubaliana na nyinyi jinsi siku za kwanza zinapaswa kupangwa. Ni muhimu kushiriki na kuwapo na mtoto katika kipindi hiki. Ni muhimu sana kusema kila mnapoondoka. Mwambie mtoto kuwa ni wafanyikazi katika chekechea ambao watamchunga ukiwa mbali. Hii inachangia mtoto kujihisi salama, na kupata uaminifu kwako na kwa wafanyikazi.

Chekechea nyingi zinataka mazungumzo na wazazi mara tu baada ya mtoto kuanza chekechea. Mazungumzo haya yanasaidia chekechea kujuana na mtoto vizuri. Hapa unaweza kusema kuhusu mahitaji maalum ya mtoto. Inaweza kuhusu chakula, kulala na masilahi, ni nani anaruhusiwa kumchukua mtoto, au vitu vingine chekechea inapaswa kuzingatia. Katika mazungumzo hayo, chekechea pia inapata nafasi ya kuwapatia wazazi habari muhimu.



© Marte Rosenvinge










## Habari kuhusu yaliyomo kwenye chekechea

Chekechea zote zina mpango wa mwaka unaoelezea huduma za kielimu wanazotoa. Zaidi, chekechea hutoa mara kwa mara habari kupitia barua za kila mwezi au barua za idara. Hapa mnapata mipango kuhusu nini ambayo itafanyika, na ikiwezekana tathmini ya shughuli ambazo zimefanywa. Chekechea nyingi huandika mara kwa mara kile kilichotokea wakati wa mchana kwa njia ya picha, maandishi au zote mbili. Chekechea zingine zina mawasialiano ya kidijitali za kubadilishana habari.

## Mazungumzo yasiyo rasmii

Mawasiliano mengi kati ya chekechea na wazazi yanafanyika katika mazungumzo yasiyo rasmi, kwa mfano katika ukumbi wa kupokea watoto na kuwachukua watoto. Hapo mara kwa mara huwa na watoto wengine na watu wazima pia.Ikiwa mnataka mazugumzo  ambayo hamtaki wengine wasikie, mnaweza kuomba mazungumzo ya kifaragha pahali pengine.



© Nina Honningsvåg Træet

## Mazungumzo rasmi

Mara mbiri kwa mwaka, chekechea inaalika kwenye mikutano ya lazima kuhusu maendeleo. Haya ni mazungumzo kati ya mwalimu wa chekechea na wazazi wa kila mtoto. Katika mazungumzo haya mnaweza kuzungumza pamoja kuhusu jinsi mnona mahitaji ya mtoto, ustawi na ukuaji wake. Mnaweza kuuliza chekechea iagize mkalimani kwa mikutano ya maendeleo ikiwa inahitajika.

## Mikutano ya wazazi

Mara moja au mbili kwa mwaka, chekechea inafanya mkutano pamoja na wazazi, ambapo wazazi wote wamealikwa. Katika mikutano ya wazazi wanazungumzia kuhusu maswala ya yanayogusa chekechea, na kila yeyote anaweza kushiriki na kutoa maoni yake.

## Baraza la wazazi na kamati ya ushirikiano

Baraza la wazazi lina wazazi wa watoto wote katika chekechea. Baraza la wazazi lina wajibu wa kuhimiza maslahi ya wazazi kwa jumla, na kuchangia ushirikiano kati ya chekechea na kikundi cha wazazi ili kuunda mazingira nzuri ya chekechea.

Kamati ya ushirikiano inajumuisha wazazi na wafanyikazi katika chekechea. Kamati ya ushirikiano ina wajibu wa kuhakikisha ushirikiano mzuri kati ya chekechea na nyumbani mwa watoto. Maswala muhimu ya chekechea yanashughulikiwa katika kamati ya ushirikiano. Mifano ya maswala hayo ni kama mpango wa mwaka, bajeti, mabadiliko ya aina ya uendeshaji au mpango.

# Kuhusu nyakati za kushiriki, kupeleka na kuchukua, ugonjwa na likizo katika chekechea



Picha: © Asle Bentzen

## WAKATI WA KUSHIRIKI RASMI

Kwa Kawaida chekechea hufunguliwa kutoka saa 07.30 asubuhi hadi 16.30. Baadhi ya shule za chekechea zina masaa zaidi ya kufungua. Chekechea yako itakujulisha kuhusu masaa yake ya kufungua. Nyinyi wenyewe mnachagua ni muda gani mtoto wenu atakuwa chekechea kila siku.

Mara nyingi katika chekechea huwa na shughuli tofauti, kuna matembezi, kipindi cha kuimba, vikundi vya kilugha na kucheza na shughuli zingine asubuhi. Julisha chekechea ikiwa utafika baadaye mchana. Kwa kufanya hivyo wafanyikazi wanajua ikiwa wanapaswa kusubiri mtoto, au ikiwa wanaweza kuanzisha shughuli za siku.

## Kuchukua na kupeleka mtoto chekechekea.

Wasiliana na wafanyikazi unapofika kwenye kituo cha kulelea watoto, ili mtoto apokelewe kwa njia nzuri. Ongea na wafanyikazi pia wakati unapofika kumchukua mtoto, na uwajulishe unapoondoka chekechea. Hii ni muhimu kwa usalama wa mtoto, na kwa kubadilishana habari kuhusu mtoto.

Ni muhimu kwamba chekechea inajulishwa ikiwa wengine kuliko nyinyi wazazi watakuja kumchukua mtoto. Kwa kufanya hivyo chekechea inaweza kutayarisha mtoto kujua. Chekechea pia hairuhusiwi kumpatiana mtoto kwa wengine bila kukubaliana mapema, hata ikiwa mtoto anamtambua mtu fulani.



© Trude Haugen






## Likizo na siku za kupumzika

Kuna wiki nne bila malipo kwa mwaka. Siku tano kati ya hizi ni siku za kupanga, wakati huo watoto wana muda wa kupumzika. Wiki zingine tatu ni za nyakati za likizo.

Baadhi ya chekechea hufunguliwa wakati wote wa majira ya kiangazi, zingine hufungwa wiki mbili/tatu kwa ajili ya likizo. Mara nyingi Chekechea huomba wazazi waripoti ni lini mtoto atakuwa na likizo ya majira ya kiangazi. Wakati mtoto ameripoti kwamba atakuwa na likizo, hawezi kuja kwenye chekechea.

Ikiwa mtoto atakuwa na muda wa kupumzika zaidi ya wiki za likizo ambazo zimekubaliwa, ni lazima mjulishe chekechea.

Chekechea huwa zimefungwa wakati wa siku kuu na pia tahere 17. mai kila mwaka, wakati wa krismasi, pasaka na likizo ya msimu wa vuli na msimu wa baridi. Kuna chekechea nyingi ambazo huuliza wazazi ikiwa watoto watakuwa likizo, ili waweze kupanga utaunzaji na wafanyakazi katika chekechea.

## Ugonjwa

Ikiwa hali ya afya kwa jumla ya mtoto ni mbaya, anapaswa kukaa nyumbani bila kushiriki kwa chekechea. Hali mbaya ya jumla inaweza kuwa uchovu usio wa kawaida, kichefuchefu, uchovu au hamu mbaya ya chakula. Watoto ambao wanatapika na kuhara, wanapaswa kukaa nyumbani siku mbili baada ya dalili kwisha, hata ikiwa hawana homa.

Sababu muhimu zaidi ya kuweka watoto nyumbani ni kuzuia kuenea kwa maambukizo katika chekechea. Hata hivyo mtoto mgonjwa anahitaji huduma ziada, na chekechea hawana uwezo wa kutoa mfanyakazi mmoja kumchunga mtoto huyo.

Ni lazima upigie simu ckekechea na uwaambie ikiwa mtoto ni mgonjwa. Hii ni muhimu sana ikiwa mtoto amepata ugonjwa ambao anaweza kuambukiza wengine.

# Dawa

Wakati mwingine watoto wanahitaji dawa ili kupona kutokana na ugonjwa. Kimsingi wazazi ndio wana jukumu la kuhakikisha kuwa dawa inapewa kwa njia sahihi na kwa wakati unaofaa, kulingana na uamuzi wa daktari. Chekechea haiwezi kulazimishwa kupeana dawa, lakini kwa kawaida wanasaidia kupatia dawa kulingana na ugonjwa. Hii lazima kukuwe makubaliano na chekechea.

Watoto wengine wanahitaji dawa kila siku kwa sababu ya ugonjwa sugu au wa muda mrefu. Ikiwa chekechea inapaswa kupeana dawa hizo, ni lazima kuwe na makubaliano maalum. Wafanyakazi lazima wapewe mafunzo kuhusu utaratibu muhimu kuhusiana na dawa hizo.



© Trude Haugen

# Kuhusu chakula na saa za chakula katika chekechea




Picha: © Asle Bentzen

# CHEKECHEA INAPASWA

- kuhakikisha kuwa kuna chakula chenye afya kila siku - iwe ni chakula kilicholetwa au chakula kilichotengenezewa chekechea

- kuhakikisha kuwa chakula na upishi wa chakula vinachangia kulete furaha ya kula, ushiriki, mazungumzo na hisia za kijamii miongoni mwa watoto

- kuwapatia watoto uzoefu wa ladha tofauti

- kuwapatia watoto maji na maziwa nyepesi au laini kama kinywaji kwa milo

- kuhakikisha kwamba watoto wanapewa maji kama wana kiu wakati katikakati ya milo

- kuhepuka vyakula na vinywaji vyenye sukari nyingi iliyoongezwa

- kuhakikisha usafi wa mikono, haswa wakati wa kula







© Trude Haugen

# CHAKULA

Katika chekechea, mtoto anaweza kula kifungua kinywa, chakula cha mchana na chakula cha matunda.

## Kiamsha kinywa – Chakula cha asubuhi

Watoto wanaofika mapema katika kituo cha kulelea watoto wanaweza kula kiamsha kinywa ikiwa wazazi wanapenda. Katika chekechea nyingi watoto wanajiletea chakula kwa pakiti ambacho wanakulia huko. Pakiti hio inapaswa kuwa na chakula chenye afya na chenye kushibisha, na ikiwezekana vipande vichache vya mboga mbichi iliyokatwakatwa. Hepuka chakula chenye sukari nyingi. Watoto wanapewa maziwa au maji kwa kiamsha kinywa.

## Chakula cha mchana

Katika chekechea nyingi, chakula cha mchana hulipwa kupitia pesa ya chakula ambayo wazazi hulipa kila mwezi. Baadhi ya chekechea zinaweza kuwa na mipango mingine. Utapokea habari kuhusu hii katika chekechea yako. Chekechea inaandaa chakula cha mchana moto au baridi kwa watoto. Chakula cha mchana kwa kawaida huwa baridi na mara nyingi ni vipande vya mkate ambavyo hubandikwa viungo tofauti na watoto wakisaidiwa na watu wazima. Chakula cha mchana moto kinaweza kuwa supu au chakula kingine chepesi cha jioni. Watoto wanapewa maziwa au maji kwa chakula hiki.

## Chakula cha matunda

Chekechea nyingi zina chakula cha matunda kila siku. Kwa kawaida kila mtoto huleta tunda moja. Matunda hayo yanakatwakatwa na kuwekwa pamoja ili kila mtu aonje kila kitu. Watoto wengine wanapenda kula chakula chao cha mchana kilichobakia, au yoghurt, kuhusiana na chakula cha matunda. Watoto wanakunywa maji pamoja na chakula.

## Chakula cha kwenda matembezi

Matembezi ni sehemu ya huduma zinazotolewa katika chekechea. Kwa kawaida mtoto lazima alete pakiti ya chakula chake cha mchana kwenye ziara za matembezi. Ni muhimu kwamba chakula cha matembezi hakihitaji kupashwa moto au maandalizi maalum. Vipande vya mkate na viungo vingine vya kubandika ni mbadala mzuri. Jisikie huru kuleta mboga zilizokatwa au matunda pia. Wafanyakazi katika chekechea wanaweza kukupa ushauri juu ya chakula cha kwenda matembezi.

## Mengine

Lazima uwajulishe wafanyikazi ikiwa kuna kitu au chakula chochote ambacho mtoto wako hali. Hii inaweza kuwa kwa sababu za kidini, kitamaduni au kiafya.


© Asle Bentzen

# Kuhusu nguo kwenye chekechea



Picha: © Nina Honningsvåg Træet

# NGUO

Katika chekechea, mtoto anapaswa kuvaa nguo ambazo hamuogopi kama zinaweza kuchafuliwa au kuharibiwa. Nguo zinapaswa kuwa rahisi kuvaa na kuvua, na starehe kwa mtoto akicheza na kutembea. Huku Bergen, kuna mvua nyingi na hali ya hewa hubadilika mara kwa mara, na inaweza kuwa vigumu kuwavalisha watoto sawa. Watoto hawapaswi kuganda juu ya baridi, lakini wanashughulika nje na hawapaswi kuvaa nguo nyingi sana ambazo zinazuia kucheza na kutumbea huru. Wafanyikazi katika chekechea wanaweza kukusaidia kuchagua nguo ambazo zinafaa kulingana na hali za hewa tofauti.

## Uwekaji wa alama kwenye nguo

Ili kuhakikisha kuwa mtoto ameleta nguo sawa nyumbani, unapaswa kuweka alama ya majina kwa nguo zote. Vitambulisho vya majina ambavyo vinabandikwa upande wa ndani ya nguo vinaweza kuagizwa kwa mtandao. Nguo zinaweza pia kuwekwa alama kwa kutumia kalamu ya wino kuzuia maji isifute.

## Je! Mtoto anahitaji nguo gani huko chekechea?

Mtoto anahitaji nguo za mvua na buti wakati kunanyesha au kuna mvua nyingi nje. Ni muhimu kuwa na seti ya nguo za mvua zilizoanikwa kwenye chekechea. Ikiwa nguo za mvua zimechafuka, zinapelekwa nyumbani na kuoshwa.

Ni lazima mtoto avae viatu vya ndani au sandale kila siku. Sakafu inaweza kuwa yenye utelezi na mtoto anaweza kuteleza ikiwa anatembea kwa soksi. Inaweza pia kuwa maji kwenye sakafu, na mtoto anaweza kupata maji kwa miguu ikiwa havai viatu vya ndani au sandale.



© Trude Haugen



© Trude Haugen



© Trude Haugen



© Nina Honningsvåg Træet

## Nguo za ziadi

Ni kawaida kuwa watoto hulowa maji au kupata uchafu wanapocheza katika chekechea. Kwa hivyo watoto wanahitaji kubadilisha nguo. Ni muhimu kuwa na nguo za ziada zilizowekwa huko chekechea, kama vile chupi, soksi, suruali ndefu ya ndani, sweta na suruali. Angalia mara kwa mara ikiwa mtoto ana kile kitu kinachohitajika kwa nguo za ziada.

## Katika msimu wa joto

Wakati hali ya hewa inakuwa joto, mtoto anahitaji nguo nyepesi na viatu vyepesi. Katika msimu wa chemchemi au vula inafaa kuvaa kofia nyembamba na ikiwezekana mavazi ya bustani bila sufu. Wakati kuna jua kali nje, mtoto anapaswa kuleta mafuta ya kujikinga kwa jua kali. Zaidi, inashauriwa kuvaa kofia ya jua au kofia ya kulinda kichwa.



© Trude Haugen



© Marte Rosenvinge

## Katika msimu wa baridi

Wakati kuna baridi nje, mtoto anahitaji suti ya baridi. Ndani ya suti hiyo anaweza kuvaa sweta na suruali ya sufu au ngozi. Vinginevyo, ni muhimu kuwa na kofia ya joto, soksi za sufu, viatu vya joto na visivyoingiza maji, na kinga za baridi za mikono.

Kumbuka kwamba mara nyingi kinga za mikono hulowa maji, kwa hivyo unaweza kuleta kadhaa.

## Mavazi wakati mtoto analala nje kwenye gari ya kumsukuma

Watoto wadogo wanahitaji kupumzika wakati wa mchana. Katika chekechea zingine, watoto wanalala nje kwa gari ya mtoto kwa usimamizi wa wafanyikazi. Ni muhimu kuwa na begi la gari, ili mtoto asivae nguo nyingi. Ndani ya begi la gari, ni vizuri kuweka nguo nyembamba za sufi hata ikiwa ni wakati wa baridi.

Ongea na wafanyikazi katika chekechea ikiwa una maswali yoyote kuhusu kulala kwenye gari la kusukuma mtoto

## Mengine

Watoto ambao wanaotumia nepi, pampas, mpira wa kunyonya, mafuta yoyote ya utunzaji lazima hii iwekwe katika chekechea.

BERGEN
KOMMUNE

Skipnes.no Svanemerket trykksak, 2041 0731 Picha: © Trude Haugen